**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI**

# JARABIO MAALUM

**DARASA LA VII - MEI 2019**

# MAARIFA YA JAMII (No.1)

**Muda: Saa 1:30**

**MAELEKEZO KWA WATAHINIWA**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, na D zenye maswali arobaini na tano (45)
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.
3. Soma maelekezo yote yaliyoko katika karatasi maalum ya kujibia (OMR)
4. Jaza taarifa zote katika fomu ya OMR na kwenye ukurasa wenye swali 41 - 45 katika karatasi ya maswali
5. Weka kivuli katika kila tarakimu ya namba yako ya mtihani kwenye nafasi husika katika fomu ya OMR
6. Weka kivuli katika herufi ya jibu sahihi kwa kila swali katika karatasi yako ya kujibia OMR kwa swali la 1 - 40. Kwa mfano kama jibu ni D weka kivuli kama ifuatavyo:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **[ A ]** | **[ B ]** | **[ C ]** | **[ ~~D~~ ]** | **[ E ]** |

7. Ukigundua kuwa herufi uliyoweka kivuli si jibu sahihi futa kivuli hicho kwa umakini kwa kutumia kifutio safi kabla ya kuweka kivuli katika herufi mpya.
8. Tumia penseli ya HB tu katika kujibu swali namba 1 - 40 na tumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi kujibu swali la 41 - 45
9. Simu za mkononi **"HAZIRUHUSIWI"** katika chumba cha mtihani.

**Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi**

**SEHEMU A: URAIA**

**Chagua herufi ya jibu sahihi**

1. Ulinzi na usalama katika kata ni jukumu la…………………….. [ ]
   (a) diwani (b) Jeshi la polisi ndani ya kata
   (c) Wananchi wote katika kata (d) Mgambo wa kata (e) Afisa mtendaji wa kata
2. ……………………ni mwenyekiti wa vikao vyote vya Baraza la mawaziri. [ ]
   (a) Waziri Mkuu (b) raisi wa Tanzania
   (c) Makamu wa raisi (d) Mwanasheria Mkuu wa serikali (e) spika
3. Ni alama gani ya taifa huonesha kwamba Tanzania ni nchi huru? [ ]
   (a) Bendera ya Taifa (b) Mwenge wa uhuru
   (c) Nembo ya taifa (d) fedha (e) uhuru na umoja
4. Mojawapo ya faida za ushirikiano wa kimataifa ni [ ]
   (a) Kuanzishwa kwa vyama vya siasa (b) Kuongezeka kwa umasikini
   (c) kuimarika kwa ulinzi na usalama (d) kuongezeka kwa migogoro
   (e) kuongezeka kwa wakimbizi
5. Kuna umuhimu gani wa kukuza na kuendeleza lugha ya kiswahili nchini Tanzania? [ ]
   (a) husaidia kuzuia utandawazi (b) hugawa watanzania katika makundi
   (c) kuendeleza ukabila (d) kuzuia matumizi ya lugha za kigeni
   (e) huleta umoja na ushirikiano
6. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana mamlaka ya kuteua wabunge…………………katika bunge la Tanzania. [ ]
   (a) watatu (b) kumi (c) wanne (d) sita (e) watano
7. …………………………ni mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama katika wilaya. [ ]
   (a) kamanda wa polisi wa wilaya (b) katibu tawala wa wilaya
   (c) Mwenyekiti wa Halmashauri wa wilaya (d) Mkuu wa wilaya
   (e) Mkurugenzi wa wilaya
8. …………………………ni mtendaji mkuu wa mahakama ya rufaa. [ ]
   (a) Jaji mkuu (b) Mwanasheria mkuu wa serikali
   (c) Jaji kiongozi (d) Waziri wa sheria na katiba (e) Hakimu mkazi
9. Nini lilikuwa kusudio la maboresho ya katiba ya Tanzania yaliyofanyika mwaka 1992?
   (a) kuruhusu mfumo wa chama kimoja [ ]
   (b) kuruhusu uchaguzi mkuu kila baada ya miaka mitano (c) kuteua wakuu wa mikoa
   (d) kuruhusu uraia wa nchi mbili (e) kuruhusu serikali kuhamia Dodoma
10. Kulingana na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, rais ana mamlaka yafuatayo, isipokuwa [ ]
    (a) kuteua mawaziri
    (b) kumteua spika
    (c) kuteua wakuu wa mikoa
    (d) kulivunja bunge
    (e) kutangaza hali ya hatari
11. Ni nani ana wajibu wa kutunza na kuendeleza maliasili ya Tanzania? [ ]
    (a) kila raia wa Tanzania (b) Wizara ya maliasili na utalii
    (c) Mamlaka ya hifadhi ya Taifa (TANAPA) (d) Jeshi la polisi
    (e) Jeshi la wananchi wa Tanzania (JWTZ)

12. Ni jumuiya ipi ina makao makuu yake mjini Gaborone Botswana? [ ]
(a) UN (b) Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)
(c) Jumuiya ya nchi za kusini mwa Afrika (SADC)
(d) Umoja wa Afrika (AU) (e) EU

**SEHEMU B: HISTORIA**

**Chagua herufi ya jibu sahihi**

13. Kazi kubwa iliyofanywa na vitangulizi vya ukoloni ilikuwa [ ]
(a) kuanzisha biashara ya utumwa
(b) kukuza viwanda vya Afrika (c) kukuza na kuendeleza Elimu Afrika
(d) kuandaa mazingira ya ukoloni (e) kukuza utamaduni wa Afrika

14. Ni jamii gani ilikuwa maarufu katika biashara kwa kutumia njia ya kusini? [ ]
(a) Wahehe (b) Wayao (c) Wanyamwezi
(d) Wakamba (e) Wamakonde

15. Gavana wa kiingereza aliyekabidhi uhuru wa Tanganyika alikuwa…………….. [ ]
(a) Richard Turnbull (b) Horace Byatt (c) Edward Twinning
(d) Julius Von soden (e) Donald Camerun

16. Michoro ya mapangoni nchini Tanzania hupatikana huko………………….. [ ]
(a) Isimila (b) Bonde la olduvai (c) Kondoa-Irangi (d) Bagamoyo (e) Zanzibar

17. Nchi za Zambia, Malawi , Ghana na Tanganyika zilipata uhuru kwa njia ya ……….[ ]
(a) Mapinduzi (b) Vita (c) Maandamano
(d) Migomo (e) Katiba

18. Vita ya MAU MAU nchini Kenya ilipiganwa dhidi ya wakoloni gani? [ ]
(a) Waingereza (b) Wareno (c) Wajerumani (d) Wafaransa (e) Waitaliano

19. Vita ya pili ya dunia ilipiganwa mwaka……………………. [ ]
(a) 1922-1945 (b) 1939-1945
(c) 1914-1918 (d) 1905-1907 (e) 1895-1905

20. Ni mwaka gani Vasco Da Gama alifika Bara Hindi (India)? [ ]
(a) 1488 (b) 1813 (c) 1904 (d) 1498 (e) 1822

21. Kiongozi mkuu wa Jumuiya ya Madola ni……………………….. [ ]
(a) Waziri mkuu wa Uingereza (b) Katibu mkuu wa Jumuiya ya madola
(c) Malkia wa Uingereza (d) Katibu mkuu wa umoja wa Mataifa
(e) Rais wa marekani

22. …………………….ni chanzo kikongwe Zaidi cha kupata habari za kihistoria [ ]
(a) Masimulizi (b) Jumba la makumbusho
(c) Maandishi (d) Maeneo ya kihistoria (e) kaboni 14

23. Soko kuu la watumwa Afrika Mashariki lilikuwa huko. [ ]
(a) Zanzibar (b) Bagamoyo (c) Mombasa
(d) Kilwa (e) Malindi

24. Kabaka alikuwa kiongozi mkuu wa falme ya …………………….. [ ]
(a) Soghai (b) Unyanyembe (c) Buganda
(d) Mali (e) Bunyoro

25. Ni wakoloni gani walitumia mfumo wa utawala wa kulisha kasumba Afrika? [ ]
(a) Wajerumani
(b) Wahispania (c) Waingereza
(d) Wadachi (e) Wafaransa

26. Kiongozi mzalendo aliyeongoza nchi ya Ghana kupata uhuru wake alikuwa……… [ ]
(a) Mnandi Azikiwe (b) Keneth Kaunda
(c) Kamuzu Banda (d) Kwame Nkurumah (e) Patrice Lumumba

**SEHEMU C: JIOGRAFIA**

**Chagua herufi ya jibu sahihi**

27. ………………ni kitendo cha kutumia taka kutengeneza bidhaa inayofaa kwa matumizi.
(a) Uvunaji wa taka (b) Ukusanyaji wa taka [ ]
(c) Matumizi mrudio wa taka (d) Utupaji wa taka (e) Utunzaji wa taka

28. ……………….ni taasisi inayohusika na utunzaji wa Mazingira Tanzania. [ ]
(a) NEMC (b) BOT (c) SUMATRA (d) TRA (e) TANESCO

29. Ukanda wa tabia ya nchi ya Ki-Ikweta hupatikana kati ya
Latitudo…………Kaskazini…………Kusini [ ]
(a) $10^0$-$15^0$ (b) $0^0$-$5^0$ (c) $5^0$-$10^0$ (d) $15^0$-$20^0$ (e) $20^0$-$25^0$

30. Mikoa maarufu kwa kilimo cha pamba nchini Tanzania ni:- [ ]
(a) Kigoma na Tabora (b) Singida na Mtwara (c) Mbeya na Iringa
(d) Shinyanga na Mwanza (e) Tanga na Kilimanjaro


31. Ni mwezi gani jua huwa la utosi kwenye tropiki ya kansa? [ ]
(a) January (b) Septemba (c) Machi
(d) Juni (e) Desemba

32. Chanzo kikuu cha nishati katika mfumo wa jua ni ……………………. [ ]
(a) Sayari (b) Jua (c) Mwezi (d) Umeme (e) Nyota

33. ……………………ni chombo kitumikacho kupima unyevu. [ ]
(a) kipima joto (b) Barometa (c) Anemometa
(d) Kipima mvua (e) Haigrometa

34. Milima ifuatayo ni yenye asili ya volkano isipokuwa ………………………….
(a) Elgon (b) Kilimanjaro (c) Kenya (d) Ruwenzori (e) Oldonyo Lengai

35. Mchoro ufuatao unaonesha ………………….. [ ]
(a) Mchoro mkato
(b) Ramani ya kisima
(c) Mistari ya mkato
(d) Ramani ya kontua
(e) Mchoro wa mlima




36. Katika mchoro hapo juu herufi A huwakilisha umbile gani la sura ya nchi? [ ]
(a) Uwanda wa juu (b) Kilele cha mlima (c) Kigongo
(d) Bonde (e) Genge

37. Nini tofauti ya muda uliopo kati ya Afrika Mashariki na nchi ya Ghana? [ ]
(a) Masaa manne (b) Masaa mawili (c) Masaa matatu
(d) Masaa matano (e) Dakika 45

38. Mabwawa ya Nyumba ya mungu na Hale hupatikana kwenye mto gani? [ ]
(a) Mto pangani (b) Mto Rufiji (c) Mto Ruvuma (d) Mto Ruvu (e) Mto Tana

39. Ni sayari gani hutumia muda mfupi zaidi kuzunguka Jua? [ ]
(a) Dunia (b) Utaridi (c) Sumbula (d) Zebaki (e) Sarateni

40. Mistari ya Meridiani hukutana wapi? [ ]
(a) Ikweta (b) Griniwichi (c) Kwenye mstari wa tarehe wa kimataifa
(d) Katikati ya dunia (e) Ncha za kusini na kaskazini mwa dunia

**Mkoa**______________________________ **Wilaya**_______________________________________

**Shule**__________________________________________________________________________

**Namba ya Mtahiniwa**__________________________________________________________

**Somo**___________________________________________________________________________

**SEHEMU D: Jibu maswali yafuatayo.**

41. Amiri jeshi mkuu wa majeshi ya ulinzi na usalama nchini Tanzania

    ni…………………………………………………………………..……………………

42. …………………………………………..………………..ni taifa la kibeberu lililoongoza katika harakati za

    kukomesha biashara ya utumwa.

43. Sekta kuu ya uchumi wa kikoloni ilikuwa ni ……………………………………….…………………………..

44. Nini umbali halisi kati ya vituo A na B kama umbali katika ramani ni sm 15, na kipimo cha

    ramani ni 1:100,000?.........................................................................

45. Tafuta jotoridi la Mbeya – Tanzania iliyopo mita 1600 kutoka usawa wa bahari, ikiwa

    Mtwara iliyopo usawa wa bahari kuna jotoridi la sentigredi $32^0$……………………………………..